

## MKATABA WA UPANGAJI OFISI

MKATABA HUU wa Upangaji Ofisi umefanyika leo hii tarehe 01 mwezi 01, 2024

### **KATI YA**

**JAMAL ALLY HASSAN** wa S.L.P. 21419, Dar es salaam (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "MPANGISHAJI") kwa upande mwingine

### **NA**

**MASS MOVERS LOGISTICS COMPANY LIMITED** ya S.L.P. 12037, Dar es salaam (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama "MPANGAJI") kwa upande mmoja;

### **AMBAPO:**

1. **MPANGISHAJI** ni mmiliki halali wa jengo lililopo ,katika Wilaya ya Kinondoni, Kata ya Kitonyama,Mkoa wa Dar es Salaam.
2. **MPANGAJI** kwa hiari yake mwenyewe amekubali kupanga Ofisi katika jengo tajwa hapo katika Kifungu Na. 1,

**KWA HIYO BASI**, pande zote mbili zimekubaliana upangaji wa Ofisi hiyo na utafanyika katika Kifungu Na. 1

1. Kodi kwa mwezi itakuwa ni Shilingi Laki Tano (Tshs. 500,000/=) tu kwa mwezi.
2. **MPANGAJI** amemlipa **MPANGISHAJI** kodi ya miezi sita (6) ambayo ni sawa na Shilingi Milioni tatu (Tshs. 3,000,000/=) tu wakati wa kusaini mkataba huu.
3. Kwa kusaini mkataba huu, **MPANGISHAJI** amekiri kupokea fedha taslimu kama pango la Ofisi hiyo kwa miezi sita (6) kiasi cha Shilingi Milioni tatu (Tshs. 3,000,000/=) taslimu.
4. **MPANGISHAJI** hatambughudhi **MPANGAJI** wala kumsumbua kwa kipindi chote cha upangaji isipokuwa endapo pale Mpangaji atakapokuwa amekwenda kinyume na kuvunja masharti ya mkataba.
5. Mpangaji atahakikisha anaitunza Ofisi anayopanga bila kuharibu ujenzi wake na kuhakikisha inakuwa katika hali nzuri kipindi chote cha Mkataba.

6. Mkataba huu utadumu kwa Miezi Kumi Na Mbili (12) toka tarehe ya kusainiwa na unaweza kuongezwa muda mwengine endapo pande zote zitaridhiana.

**KWA KUTHIBITISHA** makubaliano haya, pande zote mbili zimetia saini kama ifuatavyo:-

**MPANGISHAJI:**

**JINA** : JAMAL ALLY HASSAN

**SAINI** : 

**TAREHE** : 01/01/2024


**MPANGAJI:**


**JINA** SAAD KASSIM MAJALIWA  
Kny MASS MOVER LOGISTICS COMPANY LIMITED

**SAINI** : 

**TAREHE** : 01/01/2024

**USHUHUDA WA WAKILI:**

**JINA** : 

**SAINI** : 

**ANUANI** : Box 10559 D.D.J

**CHEO** : Wakilii

**TAREHE** : 09/1/2024

